CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MAOMBI YA MICHANGANUO YA MIRADI YA UHIFADHI WA MISITU KATIKA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI NA UKANDA WA PWANI.

UTANGULIZI

Hazina ya Mazingira Yaliyo Katika Hali ya Kuangamizwa - Critical Ecosystem Partnership Fund (CEPF) yenye makao yake makuu nchini Marekani inakaribisha michanganuo (andiko) kwa miradi ya uhifadhi mazingira na kupunguza umasikini toka kwa vikundi vya kijamii vinavyojihusisha na utunzaji wa mazingira katika misitu ya milima ya tao la Mashariki na ukanda wa Pwani. Maombi haya yanakaribishwa kufuatia mfuko wa CEPF kutoa kiasi cha dola za Kimarekani 400,000 kusaidia jamii kupata misaada ya kuendeleza jitihada za uhifadhi wa bioanuwai.

Hazina ya CEPF ni juhudi za pamoja zinazojumuisha shirika la Conservation International, Mfuko wa Kimataifa wa Kuhifadhi Mazingira (GEF), Serikali ya Japan, John D. and MacArthur Foundation, na Benki ya Dunia kwa lengo la kusaidia vikundi visivyo vya Kiserikali (Non-Governmental Organization) na vikundi vya kijamii katika jitihada za kuhifadhi maliasili za dunia hususani viumbe walio hatarini kutoweka.

WARATIBU WAKUU WA JITIHADA ZA CEPF KWA AFRIKA MASHARIKI

Shughuli zote zinazotekelezwa na mfuko wa CEPF kwa upande wa Kenya na Tanzania, zinasimamiwa na waratibu wafuatao:

1. Kitengo cha Kuhifadhi Misitu ya Ukanda wa Pwani (CFCU)
2. Shirika la Maliasili la Nature Kenya
3. Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG)
4. Shirika la Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira Tanzania (WCST)
5. Mfuko wa Kuhifadhi Maliasili Duniani (WWF)

MAENEO YATAKAYOHUSIKA

Mradi wa CEPF hapa Afrika Mashariki unalenga misitu ya milima ya tao la Mashariki na ukanda wa Pwani. Eneo hili kwa Tanzania linajumuisha wilaya za Mwanga, Same, Lushoto, Muheza, Korogwe, Kilindi, Mvomero, Kilosa, Mpwapwa, Kilolo, Mufindi, Morogoro, Kilombero, na Ulanga. Eneo la Pwani linajumuisha mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Dar es Salaam,Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

Miradi itakayopewa kipaumbele katika kupatiwa ufadhili ni ile itakayolenga kutatua matatizo ya jamii katika jitihada zao za kuhifadhi bioanuwai. Vigezo muhimu ni pamoja na kuhakikisha miradi inalenga:

- Kuchangia uhifadhi wa misitu ya ukanda wa Pwani na ile ya Tao la milima ya Mashariki.
- Kusaidia kuhifadhi bioanuwai iliyo hatarini kutoweka
- Shughuli za kupunguza umasikini na ambazo hazichangii uharibifu wa mazingira
- Ushirikishwaji wa wananchi hususani wanawake na vijana.
- Kuonyesha uwazi katika usimamizi na matumizi ya fedha
- Shughuli za uhamasishaji na elimu ya mazingira

NANI ANAWEZA AU KUSTAHILI KUOMBA

Ili kupata msaada wa CEPF, mwombaji inabidi iwe ni asasi au kikundi cha kijamii kinachotambulika na serikali ya Kata, Kijiji au mtaa wa eneo husika. Waombaji wanaweza kuwa ni serikali ya kijiji, kikundi cha watu, asasi binafsi inayofanya kazi ngazi ya kijiji, tarafa au wilaya. Asasi au Kikundi husika lazima kiwe na uzoefu wa mwaka mmoja au zaidi. **Na pia kiwe na shughuli inayoendelea katika eneo husika.**

Tanzania Forest Conservation Group

WCST

WWF for a living planet

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MAMBO MUHIMU YATAKAYOZINGATIWA WAKATI WA KUCHAGUA MIRADI

Katika kuchagua miradi itakayopewa usaidizi, Kamati ya kuratibu itazingatia zaidi miradi ambayo inalenga KUHIFADHI VIUMBE WALIO HATARINI KUTOWEKA (critically endangered species). Na pili kipaumbele kitatolewa kwa mradi/miradi inayolenga kuhifadhi misitu.

Mambo mengine yatakayozingatiwa katika kuchagua miradi ni pamoja na:

1 Jinsi mradi utakavyochangia uhifadhi wa bioanuwai kwa mfano utakavyosaidia kupunguza matumizi ya maliasili.
2 Jinsi jamii husika itakavyoshirikishwa.
3 Jinsi mradi utakavyokuwa endelevu

Mambo ambayo CEPF haitatoa msaada ni pamoja na:

4 Ununuzi wa gari, nyumba, au shamba
5 Mishahara
6 Shughuli za kiserikali
7 Kuhamisha watu kwenye maeneo yao kwa nguvu
8 Kubadilisha hali ya uasilia wa mazingira ya eneo fulani.

KIASI CHA FEDHA (MSAADA) KINACHOWEZA KUOMBWA/KUTOLEWA

Miradi itakayosaidiwa na CEPF kupitia fungu hili la kusaidia vikundi vya kijamii ni ile miradi inayoomba kiasi cha fedha kisichozidi million mbili (2,000,000). Muda wa mradi unaweza kuwa miezi sita hadi mpaka mwaka mmoja na nusu. Maombi kwa miradi isiyozidi milioni tano (5,000,000) yanaweza kuwasilishwa ingawa nafasi ya kupewa msaada ni finyu (ndogo).

LINI UNAWEZA KUWASILISHA MAOMBI?

Maombi ya michanganuo ya mradi yatapokelewa wakati wowote kuanzia sasa hadi mwaka 2008. Kamati ya uratibu itakaa kila baada ya miezi mitatu kuchambua na kupitisha maombi yaliyopokelewa.

JINSI YA KUOMBA

Maulizo na michanganuo ya miradi yapitishwe kwa mojawapo ya asasi zinazounda kamati ya uratibu ambazo ni CFCU, Nature Kenya, TFCG, WCST na WWF au yanaweza kutumwa moja kwa moja kwa njia ya nukushi au posta kutumia anwani ifuatayo:

Mwakilishi Mkazi
WWF Tanzania Programme Office,
Plot 350 – Regent Estate Mikocheni,
S.LP. 63117
DAR ES SALAAM (TZ)

Simu: +255 (0) 22 270 0077
Nukushi: +255 (0) 22 277 5535
Barua Pepe: JSalehe@wwfearpo.org

WOTE MNAKARIBISHWA KULETA MCHANGANUO WA MRADI.

Tanzania Forest Conservation Group

WCST

WWF for a living planet

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

JAZA FOMU YA MAOMBI

Jina kamili la Mradi (Mfano: Mradi wa Ufugaji Nyuki wa Kisasa katika kijiji cha Nzasa, Wilaya ya Temeke.)		
Jina kamili la asasi au Kikundi kinachoomba:		Eleza kama una usajili wa ngazi yoyote:
Tarehe:		Jina kamili la msimamizi mkuu wa mradi:
Eneo mradi utakapotekelezwa:		Anuani kamili ya mwombaji: S.L.P: _____ Simu: _____ Barua pepe (kama ipo): _____

ELEZA KWA UFUPI NI KWANINI MRADI KAMA HUU UNAHITAJIKA KATIKA ENEO HUSIKA

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

TAJA MALENGO YA MRADI (Mfano: Kupata asali kwa ajili ya chakula na kuuza ili kupunguza umasikini)

1.
2.
3.
4.
5.

TAJA SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA (Mfano: Kutengeneza mizinga ya kisasa; kutafuta masoko)

1.
2.
3.
4.
5.

TOA MAELEZO MAFUPI YA JINSI KILA SHUGHULI ITAKAVYOTEKELEZWA

ELEZA KWA UFUPI JINSI MRADI HUU UTAKAVYO ISAIDIA JAMII (Mfano:Kupunguza umasikini na ukataji miti)

1.
2.
3.
4.
5.
6.

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MATOKEO (MANUFAA) YANAYOTARAJIWA (Mfano: Matumizi endelevu ya misitu)

1.
2.
3.
4.
5.

JE? UNA SHUGHULI YOYOTE UNAOYOFANYA KWA SASA KATIKA SUALA NZIMA LA UTUNZAJI WA MAZINGIRA? Kama ipo toa maelezo mafupi kuelezea mahali na shughuli yenyewe

MUDA WA UTEKELEZAJI WA MRADI

Muda:_____ Tarehe ya Kuanza: _____ Tarehe ya Kumalizika: _____

MPANGO WA KAZI

	SHUGHULI	MUDA WA UTEKELEZAJI	WAHUSIKA
1.			
2.			
3.			
4.			
5.			
6.			
7.			
8.			
9.			

CRITICAL ECOSYSTEM PARTNERSHIP FUND

MWONGOZO WA BAJETI

SHUGHULI	KIASI CHA FEDHA	MAELEZO MAFUPI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
	JUMLA	
	KIASI KINACHOOMBWA	
	MCHANGO TOKA KWA WENGINE	
	MCHANGO USIO WA FEDHA TASLIM	

1. Toa maelezo mafupi kama una tarajia kupata fedha toka kwa ufadhili mwingine zaidi ya huu.

2. Je? Unayo akaunti ya benki? Ndiyo/Hapana_____Itaje_____

UTAMBULISHO

Maoni na utambulisho toka kwa ofisa wa Kata au Mtendaji wa Kijiji wa eneo husika:

Jina la Kiongozi_____Cheo: _____

Maoni_____

_____

_____

Sahihi: _____ Tarehe: _____

(Piga Muhuri hapa)

SAHIHI YA MWOMBAJI

Jina:_____Sahihi: _____

Tarehe: _____

Tanzania Forest Conservation Group

WCST

WWF for a living planet